# KONGAMANO LA WAANGALIZI WA HAKI ZA ARDHI VIJIJINI - GWATA UJEMBE

*05 Agasti 2023*

*+255 784 646 752*



Waangalizi wa haki za ardhi vijijini walifanya kongamano la kuadhimisha sikukuu ya wakulima nchini katika kijiji cha Gwata Ujembe wilaya ya Morogoro kusini mkoani Morogoro. Kongamano hilo lilikua na mada mbalimbali zikiwemo, migogoro ya ardhi na upatikanaji wa chakula vijijini, athari za mabadiliko ya tabianchi katika mifumo endelevu ya chakula, ulinzi wa haki za ardhi za wanawake ni msingi imara wa mifumo endelevu wa chakula, utunzaji wa mazingira kwa uzalishaji wenye tija na mikopo ya kausha damu inavyo wadidimiza wakulima wadogo vijijini. Yafuatayo ni masuala yalioibuka katika uwasilishwaji wa mada hizi.

## UTANGULIZI



**UFUNGUZI:** Afisa programu wa Taasisi ya Hakiardhi, Bi. Happiness George akiendesha ratiba ya kongamano la Waangalizi wa Haki za Ardhi vijijini lililokuwa na kaulimbiu ikisema **"Vijana na Wanawake ni Msingi Imara wa mifumo endelevu ya chakula"**. Hivyo Waangalizi walijikita kikamilifu katika uwasilishaji wa mada zao.



**LENGO:** Mwenyekiti wa Waangalizi wa haki za ardhi vijijini Bw. Omari Kindamba, akitoa lengo na madhumuni makuu ya kongamano la kuadhimisha sikukuu ya wakulima nchini (Nanenane). Pia kwa moyo mkunjufu aliwakaribisha wageni wote wakiwemo Diwani, Mwenyeki na Mtendaji wa Gwata Ujembe, wafanyakaazi wa Taasisi ya Hakiardhi na wengine wote walioshiriki kongamano hilo.

# MASUALA YALIYOIBUKA



**MIGOGORO YA ARDHI NA UPATIKANAJI WA CHAKULA:** Muangalilizi wa haki za ardhi Richard Nehemia, kutoka kijiji cha Chita - Kilombero alito muhtasari kuhusu migogoro ya ardhi kwa alichangia uzoefu kutoka kijijini kwake. Mwangalizi huyu akiambatana na Mustapha Jongo kwa pamoja walisema kwamba kupitia mafunzo toka Taasisi ya Hakiardhi walifanikiwa kufungua zaidi ya madarasa saba na kuingia kwenye harakati za kupambania ardhi yao iliyochukuliwa na serikali ya kijiji na hatimaye baadhi ya mashamba yalirudishwa



**ATHARI ZA MABADILIKO YA TABIANCHI KATIKA MIFUMO ENDELEVU YA CHAKULA:** Mwangalizi Sadiki Hatibu aliambatana na Ahmadi Mchotama kutoka Micheka - Kilombero kwa pamoja walielezea dhana ya mabadiliko ya tabianchi. Kutokana na uzoefu wa masuala yalioibuka katika vijiji vyao walieleza kwa jinsi gani athari za mabadiliko ya tabianchi huathiri mifumo endelevu ya chakula. Masuala hayo yalikua ni pamoja na, kufifia kwa vyanzo vya maji, uhaba wa mvua na kukauza kwa uoto wa asili. Athari hizi hufanya chakula kua haba na hatimaye mifumu ya chakula kua sio endelevu.



**UKATILI WA KIJINSIA**: Mwangalizi wa haki za ardhi kutoka Msamvu - Kilindi, Bi Mwamini Botto alitoa muhtasari kuhusu masuala ya ukatili wa Kijinsia. Katika muhtasari wake alijikita zaidi katika kuzungumzia masuala ya ubakaji na ulawiti wa watoto wadogo. Kwa uzoefu alioupata katika kijiji chake masuala ya ulawiti wa watoto wadogo umeshamiri, hivyo alisisitiza wazazi na walezi kuchukua tahadhari kwa kuwaweka mbali watoto wao na watu wasio wafahamu ili kuwaepusha na matatizo ya ubakaji na ulawiti.



**MASOKO:** Mwenyekiti wa wangalizi wa ardhi Bw. Omari Kindamba alizungumzia kwa kina kuhusu suala la stakabadhi ghalani. Alisema kuwa mfumo wa stakabadhi ghalani ni utaratibu uliowekwa na maafisa ya serikali kwa kutojali maslahi mapana ya wakulima wadogo. Mfumo huo huendeshwa kwa kukusanya mazao ya wakulima na kuyapima kisha kuwatoza ushuru na baadae mazao hayo hupangiwa bei bila kuwashirikisha wazalishaji wa mazao hayo. Hvyo mazao hayo huuzwa kwa bei zisizo na tija kwa wakulima wadogo. Serikali inadai kwamba huo ni ushirika wa kunyanyua wazalishaji wadogo kitu ambacho ni kinyume na uhalisia.



**MBEGU:** Mwangalizi wa haki za ardhi Bw. Boniventure Mpole akitoa muhtasari kuhusu mbegu. Katika muhtasari wake alisema kuwa kwa sasa kuna changamoto kubwa katika mbegu kwani mbegu asilia zinapotea na mbegu za kisasa kuja kwa kasi. Hivyo basi wananchi wanapaswa kuwa makini katika utunzaji wa mbegu za asili kwa usalama na mifumo endelevu ya chakula.



**PEMBEJEO:** Mwangalizi wa haki za ardhi kutoka Liwale - Lindi Bw. Haji Mpacha alizungumzia namna ambavyo baadhi ya Taasisi zikishirikiana na serikali kudai kwamba zinatoa pembejeo za kilimo bure kwa wakulima kwamba ni upotoshaji. Alisema kuwa kiuhalisia bembejeo hutolewa na Taasisi hizo jambokuwa gharama zake hufidiwa katika makato mbalimbali yanayowekwa katika mchakato wote wa uzalishaji ambao wakulima wadogo hupitia mpaka kufikisha mazao yao sokoni. Alihitimisha kwamba wananchi inabidi tuamke kupinga mifumo hii kandamizi.



**MIKOPO YA KAUSHA DAMU:** Mwangalizi wa haki za ardhi kutoka Gwata Ujembe Bi. Joyce Kakwabanga akiambatana na Joyce Funi kutoka Mikese, Mtego wa Simba kwa pamoja walielezea mikopo ya kausha damu. Walisema kuwa hii ni aina ya mikopo inayokopeshwa kwa wajasiriamali wadogo hususan wakinamama na wazalishaji wengine wadogo kwa lengo la kuwanyanyua kiuchumi. Japokua kiuhalisia wake walisemakuwa mikopo hii ni kandamizi na husababisha matatizo makubwa yakiwemo, kuvunjika kwa familia, umasikini uliokithiri na hata utelekezwaji kwa baadhi ya familia.



**ULINZI WA HAKI ZA ARDHI KWA WANAWAKE:** Muangalizi wa haki za ardhi kutoka kijiji cha Dutumi, Kilosa - Morogoro, Bi. Mwajuma alitoa muhtasari wa ulinzi wa haki za ardhi kwa wanawake ni msingi imara wa mifumo endelevu ya chakula. Alieleza kuwa wanawake ndio wazalishaji wakubwa wa chakula hasa kwa kukidhi mahitaji ya kukidhi familia. Kwahiyo wanawake wanahaki ya kumiliki ardhi kwa namna na misingi ile ile kama wanaume wanavyo miliki ardhi. Hivyo mwanamke akimiliki ardhi kunkuwa na msingi imara wa mifunmo endelevu ya chakula.

# UZOEFU KUTOKA KWA WAANGALIZI MBALIMBAKI



Mkazi wa Kilosa ambae jina lake limehifadhiwa, alitoa uzoefu katika kijiji chake yakuwa, yeye na wenzake walipatiwa ardhi na serikali ya kijiji na wakaanza kutumia ardhi hiyo kwa shughuli za kawaida za kilimo. Baada ya siku chache alitokea muwekezaji aliye dai kwamba ardhi hiyo ni mali yake kisha akaenda kuwashtaki wakinamama hao kituo cha polisi. Baada ya polisi kupokea mashtaka , waliamua kwenda mara moja kuwakamata wakinamama hao na kuwaweka ndani na baada ya siku chache wakafikishwa mahakamani. Cha kusikitisha serikali ya kijiji ikawashutumu yakuwa ni wavamizi na kuzuia dhamana yeyote dhidi ya kesi hio. Hivyo wanaiomba serikali iweze kuwafikiria kwa kina na kuwapatia haki yao. Kwani ardhi hio waligawiwa na serikali ya kijiji.



Bi. Joyce Willium ni muangalizi wa haki za ardhi kutoka kijijini Kingamalucha, Nzega. Mwangalizi huyu alihadithia namna alivyofanikisha kusaidia watoto waliofanyiwa ukatili wa kijinsia, na ndoa za utotoni kurudi shuleni. Kwa moyo wake wa ushupavu na ujasiri aliweza kufatilia hatua kwa hatua kutoka ngazi za serikali ya kijiji hadi wilayani kuhakikisha kwamba watuhumiwa wanatiwa mikononi mwa serikali na watoto hao kurudi shule. Hatimaye kwa kushirikiana na afisa wa ustawi wa jamii walifanikiwa kuwasaidia watoto kurudi masomoni na watuhumiwa kuwekwa ndani.



Mwenyekiti wa waangalizi wa haki za ardhi Kilosa, Bw. Mustapha Jongo, aliwahamasisha wanakijiji wa Gwata Ujembe yakwamba, wanapaswa kuzingatia sheria jinsi inavyosema waliwa katika harakati za kudai ardhi yao kwani kutokufanya hivyo kutawapelekea kupoteza haki yao. Pia aliwausia waangaliziwenzake wapambane kwa moyo kwani viongozi wa serikali huwahonga waangalizi legevu kwa kuwapa ardhi, kitu ambacho huwapunguzia uwajibikaji hususan katika madarasa yao. Hivyo alihitimisha ya kwamba njia za mapambano ni ngumu lakini zinawezekana kama tukitia juhudi.



Mwangalizi wa haki za ardhi kutoka Vunila - Kilindi, Bw. Ramadhani Mdora akitoa uzoefu kutoka kijijini kwake yakuwa wananchi walinyang'anywa ardhi yao kwa kudai kuwa wamevamia ardhi ya muwekezaji. Pamoja na kwamba ardhi ni yao lakini wamekuwa ni waoga kudai haki yao. Hivyo alisisitiza kwamba wananchi wanapaswa kuendesha harakati za kudai haki zao bila woga kwani kufanyahivyo huleta tija kwa kuwawezesha kujikwamua kiuchumi.




Mwanachama wa Taasisi ya Hakiardhi Bi Marcelina Kibena akitoa majumuisho ya mada zote zilizowasilishwa na waangalizi wa haki za ardhi. Majumuisho hayo yalikuwa pamoja na, kuwapongeza waangalizi kwa kuweza kuandaa kongamano la kitaifa kuadhimisha sikukuu ya wakulima nchini. Alitilia mkazo yakwamba, migogoro ya ardhi vijijini hudidimiza maendeleo na kufanya upatikanaji wa chakula kuwa mgumu mno vijijini.

Pia alisema kwamba mabadiliko ya tabianchi yametokea kwa kasi zama hizi kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo, uharibifu wa mazingira hususan ukataji wa miti na kilimo cha kuhamahama na utumiaji wa kemikali katika kilimo zinazo haribu rutuba asilia ya udongo.

Ulinzi wa haki za ardhi za wanawake pia ni jambo alilotilia msisitizo kwani, wanawake ndio wazalishaji wa awali wa chakula hasa kwaajili ya kukidhi mahitaji ya familia. Hivyo kulinda haki za ardhi za wanawake hupelekea kuwa na msingi imara wa mifumo ya chakula.

Hatimaye, alimalizia kwa kuwahamasisha wananchi kutunza mazingira, kuzingatia matumizi ya mbegu asilia. Pia, alisisitiza wazazi kuwa waangalifu kwa watoto wao kwani vitendo vya ubakaji na ulavwiti vimeshamiri sana. Mwisho alitoa shukurani za dhati kwa washiriki wote waliojitokeza katika kongamano hilo na hatimaye washiriki walipata chakula pamoja na burudani ya muziki kisha machapisho yakigawiwa kwa washiriki kwaajili ya kuwaelimisha juu ya haki za ardhi.

## SHAMRASHAMRA ZA KONGAMANO








